



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA SHINYANGA



Ofisi ya Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga, SLP 113, Iselamagazi,
SHINYANGA Simu/Fax: 0282-986382 Barua pepe: info@shinyangadc.go.tz

Website: www.shinyangadc.go.tz

Unapojibu tafadhali taja:

Kumb.Na.SDC/ C.4/7/Vol.I/49

13.08.2021

TANGAZO LA NAFASI YA KAZI

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga kupitia Kibali cha Ajira mbadala chenye Kumb. Na.FA.170/376/01"B"/60 cha tarehe 19 Julai, 2021 kilichotolewa na Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora (UTUMISHI) anatangaza nafasi ya kazi kwa Wananchi wa Tanzania wenye şifa na ujuzi wa kujaza nafasi ifuatayo:-

I: Mtendaji wa Kijiji Daraja la III (Nafasi 1)

(a) Sifa za Mwombaji:

- Awe amehitimu Kidato cha Nne au Sita na Cheti cha Mafunzo (NTA LEVEL 5) katika fani mojawapo kati ya hizi; - Utawala, Sheria, Elimu ya Jamii (Sociology). Usimamizi wa Fedha, Maendeleo ya Jamii na Sayansi ya Sanaa kutoka katika Chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali.

(b) Kazi na majukumu ya Mtendaji wa Kijiji Daraja III

Mtendaji wa Kijiji atatekeleza majukumu yafuatayo.-

- Afisa Masuhuli na Mtendaji Mkuu wa Serikali ya Kijiji
- Kusimamia Ulinzi na Usalama wa Raia na Mali zao,
- Mlinzi wa Amani na Msimamizi wa Utawala Bora katika Kijiji,
- Kuratibu na kusimamia upangaji na utekelezaji wa mipango ya maendeleo ya Kijiji
- Katibu wa Mikutano Mikuu na Kamati zote za Halmashauri ya Kijiji,
- kutafsiri na kusimamia Sera, Sheria na Taratibu za Serikali katika ngazi ya Kijiji.

(c) Ngazi ya Mshahara:

- Mwombaji atakaefanikiwa kuajiriwa kwa Cheo cha Mtendaji wa Kijiji Daraja la III atalipwa mshahara ngazi ya TGS B kwa mwezi.

2: MASHARTI YA JUMLA KWA WAOMBAJI WOTE JUMLA


- (i) Waombaji wote wawe ni raia wa Tanzania na wenye umri kuanzia miaka 18-45,
- (ii) Mwombaji aliyewahi kupatikana na kosa la jinai hatafikiriwa,
- (iii) Barua ya mwombaji ioneshe anuani anayotumia kwa sasa Pamoja na namba za simu ikiambatana na:
 - a) Maelezo binafsi ya mwombaji (CV)
 - b) Nakala za vyeti vya kidato cha Nne au Sita kwa wale waliofika kiwango hicho na vyeti vya kuhitimu mafunzo mbalimbali (Taaluma) kwa kuzingatia sifa tajwa hapo juu.
 - c) Nakala ya cheti cha kuzaliwa
 - d) Picha mbili (2) za Passport Size za hivi karibuni
- e) **Kitambulisho au namba ya kitambulisho cha Taifa (NIDA)**
 - (iv) Watakaochaguliwa kuhudhuria usaili (Shortlisted Candidates) watafahamishwa kupitia anuani na namba za simu walizotumia kwenye barua zao za maombi ya kazi,
 - (v) **Testimonials na Provisional results havitakubalika,**
 - (vi) Kwa wale waliosoma nje ya Tanzania wahakikishe kwamba vyeti vyao vimehakikiwa na kuthibitishwa na Mamlaka (TCU au NECTA) kulingana na ngazi ya cheti,
 - (vii) Nakala zote za vyeti vya Shule, Chuo, kitambulisho cha Taifa (NIDA), na cheti cha kuzaliwa vithibitishwe na Wakili yeyote aliyesajiliwa na kuthibitishwa au Mahakama.

Mwombaji mwenye sifa anatakiwa kutuma maombi kupitia Posta kwa anuani ifutayo;-

Mkurugenzi Mtendaji (W),
Halmashauri ya Wilaya Shinyanga,
S. L. P 113,
SHINYANGA.

Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 27 Agosti, 2021 saa tisa na nusu alasiri.

NB:Tangazo hili pia linapatikana katika tovuti ya Halmashauri
www.shinyangadc.go.tz



Nice R. Munissy

MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA YA SHINYANGA
MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA
S.L.P. 113
SHINYANGA